



## Uridhi wa sanaa iliyochoywa katika mawe:

### Hoja muhimu

#### Je, sanaa hii ni nini na hupatikana wapi?

- Bara la Afrika lina aina mbalimbali za sanaa-mawe kuliko bara lingine lolote duniani.
- Afrika ina baadhi ya sanaa – mawe za kwanza kuwahi kuonekana. Michoro ya wanyama kwenye mawe ilichimbuliwa kule Namibia na inaaminika ilikuwa imemaliza miaka 27,000.
- Imekadiriwa kuwa kuna zaidi ya michoro na picha zilizochongwa milioni kumi barani Afrika.
- Sanaa-mawe hupatikana kwa wingi katika jangwa la Sahara, Afrika Kusini ingawa pia kuna sanaa-mawe muhimu Afrika ya Kati na Africa Mashariki.

#### Umuhimu wa sanaa hii

- Inatoa ushahidi wa kwanza kuhusu ubunifu wa binadamu.
- Ni njia moja ya awali iliyotumiwa na binadamu katika mawasiliano na kuonyesha ujuzi wake katika sanaa.
- Sanaa-mawe ni sehemu ya toradhi zetu: yaani tutaweza kujielewa na vile vile kuelewa asili yetu.
- Sanaa-mawe inatoa ushahidi kuhusu jinsi mababu wetu walivyoshugulikia maswala mbali-mbali na vile vile kutueleza asili ya imani za kisasa.

#### Je, Sanaa hii inatishwaje?

Sanaa mawe nyingi zimechuchuka na ni rahisi kuharibika. Sasa hivi inatishwa na ukuaji wa idadi ya watu, kutojali, uharibifu, wizi, utalii usiyokuwa na utaratibu mwafaka na maendeleo ya miradi ya kitaifa kama vile barabara mpya, hifadhi, upanuzi wa miji, uchimbaji madini na maendeleo ya kiviwanda. Kwa muda wa miaka hamsini zijazo, huenda kiasi kikubwa cha sanaa hii kutaharibiwa na kufanya vizazi vitakavyofuata kukosa cha kufurahia na kusoma.

#### Sanaa hii inaweza kuhifadhiwa vipi?

Ulinzi wa toradhi hii ni jambo linalohusisha kila mlimwengu. Lazima tujifunze kuelewa sanaa hii, tujaribu tukadirie umri wake, maana ya picha na sababu zilizofanya picha hizo kuchorwa. Kuelewa sanaa hii na umri wake ni dhahirisho la thamani yake. Ni jukumu la kila mtu, wewe, mimi na yeyote yule kuheshimu sanaa hii na kuihifadhi ili watoto wetu na vizazi vyao wafaidike.

Simu: +254 20 884467, 883735 | [tara@africanrockart.org](mailto:tara@africanrockart.org) | [www.africanrockart.org](http://www.africanrockart.org)



TRUST FOR AFRICAN ROCK ART